

# Kwa nini Utumie Bitcoin?

Bitcoin ni kama pesa taslimu ila ni ya kidijitali

Hauhitaji benki, ruhusa, kitambulisho, au kuwa tajiri kutumia bitcoin.

Bitcoin haiathiriki na mfufumuko wa bei, kughushi, au kusimamishwa na mtu yeyote.

Bitcoin yako ni ngumu kuiba kuliko pesa taslimu.

Malipo yako hayawezi kukaguliwa na kudhibitiwa

Bitcoin yako haiwezi kusimamishwa kama akaunti ya benki.

Kuwa na chelezo/funguo/keys (maneno 12 ya Kiingereza)

ina maana bitcoin yako ni YAKO peke yako!

## Mkoba(Wallet) wako wa Kwanza WA Bitcoin

1 - Download app - kwa mfano

"Muun" au kama inavyotumika hapa "Blue Wallet"



App Store



Google Play

2 - Ifungue na ufuate maagizo ukurasa unaofuata.

**Huu sio ushauri wa kifedha.  
Fanya utafiti wako mwenyewe!!**

# Tumia Bitcoin

Akaunti ya Akiba  
Kiasi > USD 100

## 1. Tengeneza mkoba wa Bitcoin

na chelezo/KEYS (isiyo ya uhifadhi)

Andika maneno 12 ambayo utaona kwenye skrini kwenye kipande cha karatasi.

HAKUNA picha ya skrini, HAKUNA nakala ya dijitali. Unaweza kurejesha pesa zako kwa maneno haya 12.

## 2. Pata anwani ya bitcoin

Bonyeza kitufe cha Pokea na utawasilishwa msimbo wa QR na safu ya nambari na herufi. Hii ndio anwani yako ya bitcoin, ankara.



## 3. Pokea bitcoin

Nakili na utume msimbo wa QR au safu kamili ya herufi na nambari kwa mtu anayetaka kukutumia bitcoin.

Baada ya kulipwa, mkoba wako utakujulisha kuwa malipo yamepokelewa. Malipo katika (on-chain) bitcoin inaweza kuchukua muda.

## 4. Tuma bitcoin

Bonyeza Tuma na uchanganue msimbo wa QR wa mpokeaji. Angalia na uidhinisha malipo.



# Tumia Lightning Bitcoin

Matumizi ya kila siku  
Malipo madogo ya haraka

## 1. Unda Lightning Wallet

na chelezo (uhifadhi)

Hifadhi msimbo wa QR au anwani ya Indhub. Usifichue!

Unaweza kurejesha pesa zako kwa kuchanganua msimbo wa QR katika mkoba au wallet mpya.

## 2. Unda ankara

Bonyeza kitufe cha Pokea ili kutoa ankara mpya, kisha uweke akaunti ili kupokea.

Unaweza kubadilisha kati ya sarafu ili kuona kiasi kwa bitcoin au USD.



## 3. Pokea Lightning bitcoin

Nakili na utume msimbo wa QR au safu kamili ya herufi na nambari kwa mtu anayetaka kukutumia lightning.

Baada ya kulipwa, mkoba wako utakujulisha kuwa malipo yamepokelewa. Malipo ya umeme ni ya haraka.

## 4. Tuma bitcoin

Bonyeza Tuma na uchanganue msimbo wa QR wa wapokeaji. Angalia na uidhinisha malipo.



## Miliki Pesa yako

Ukinunua bitcoin kwa Exchange, ni kama pesa kwa benki. Inaweza simamishwa; unachomiliki na unachofanya kwa pesa zako kinaweza kufuatiliwa.

Tumia bitcoin inavyoonyeshwa katika brosha hii na uitumie na familia yako, marafiki na washirika wa biashara.

Kamwe usishiriki chelezo/funguo/keys zako na mtu yeyote au zihifadhi kidijitali.

***Sio funguo(keys) zako, sio bitcoin yako.***

Matumizi

- Pata bitcoin (kazi ya mtandaoni, podcasting, michezo ya mtandaoni, kuwa msanidi programu...)
- Pokea pesa zinazotumwa (ada za chini)
- Lipa ndani na nje ya nchi (ada za chini)
- Uliza maduka ya karibu yako kukubali bitcoin
- Ibadilishe rika-kwa-rika hadi USD au sarafu ya nchi yako (uliza tume Bitcoin)

***Uliza Vikundi vya WhatsApp vya elimu***

## Bitcoin ni Nini?

Bitcoin sio utapeli

Bitcoin ni pesa za rununu zinazofanya kazi bila kampuni au serikali nyuma yake. Ni teknolojia kama mtandao.

Unaweza kumiliki sehemu za bitcoin inayoitwa satoshi. Hakuna vikomo vya miamala. Ada ni ndogo. Ushuru hauwezi kukatwa kiotomatiki.

### Jinsi ya kugundua Utapeli

Ni utapeli ikiwa unahitaji

- Mlete rafiki au mwanafamilia
- Nunua kifurushi cha kuanzia
- Fanya malipo ya kila mwezi

***Hakuna haja ya kujiunga na Bitcoin!***

Ni mtandao wazi ambao mtu yeyote anaweza kutumia bila ruhusa

- Bitcoin haiahidi faida
- Bei ya Bitcoin ni tete. Ihifadhi kwa miaka 4-5 au itumie mara moja

***Jifunze zaidi katika [www.bffbtc.org](http://www.bffbtc.org)***

# Bitcoin Pesa yako Haki yako!

Pesa ya Kidijitali

Itumie kutoka kwa mtu hadi mtu

Hakuna haja ya benki  
au usajili

Hakuna udhibiti wa shirika

Pesa za jumuiya

